TANGAZO LA SERIKALI NA. 82 la tarehe 7/2/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

## SHERIA NDOGO YA UDHIBITI WA VYOMBO VYA USAFIRI YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM YA MWAKA 2025

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2025.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"abiria" maana yake ni mtu yeyote anayesafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine;

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa, mkokoteni au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

"katikati ya Jiji" maana yake ni maeneo yote ya Kata za Mchafukoge, Kivukoni, Kisutu, Gerezani, Mchikichini, Kariakoo, Jangwani, Ilala, Upanga Magharibi, Upanga Mashariki, Kipawa, Buguruni, Mnyamani au Vingunguti na maeneo mengine yatakayoidhinishwa na Halmashauri;

"kituo cha magari ya abiria" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"maegesho" maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

"magari ya mizigo" maana yake ni magari yanayobeba mizigo yenye uzito zaidi ya tani tatu;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mtumiaji wa kituo" maana yake ni mtu yeyote anayefanya shughuli zake za kila siku ndani ya kituo na ametambuliwa na Halmashauri; na

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri.

Wajibu wa Halmashauri

**4**. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kuweka utaratibu wa usimamizi na udhibiti wa vyombo vya usafiri katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho ya magari;

(b) kutenga maeneo ya maegesho kwa kushirikiana na wadau;

(c) kuanzisha na kusimamia uendeshaji wa kituo cha magari ya abiria;

(d) kusimamia uingiaji na utokaji wa magari na mitambo katikati ya Jiji;

(e) kutoza ushuru na ada kwa watumiaji wa kituo cha magari ya abiria na abiria;

(f) kuwatambua wamiliki wa magari ya abiria kwa mujibu wa vyama au vyombo vilivyosajiliwa na kutambulika; na

(g) kuondoa na kuvuta vyombo vya usafiri vilivyoegeshwa maeneo yasiyo rasmi.

Magari na mitambo kuingia katikati ya Jiji

**5**.-(1) Magari ya mizigo, kontena, pikipiki ya magurudumu mawili au matatu, matoroli au maguta hayataruhusiwa kuingia katikati ya Jiji.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), magari ya mizigo, kontena, pikipiki ya magurudumu mawili au matatu yanaweza kuingia katikati ya Jiji baada ya kupata kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi.

(3) Kibali cha kuingia katikati ya Jiji kitatolewa baada ya kulipiwa ada na kitajumuisha kupakia na kushusha mzigo.

(4) Magari ya taka na mitambo yoyote haitaruhusiwa kuzoa au kukusanya taka au kufanya kazi katikati ya Jiji nyakati za mchana isipokuwa kwa kibali maalumu cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi.

Wajibu wa mmiliki wa chombo cha usafiri

**6**. Mmiliki wa chombo cha usafiri hataruhusiwa kuanzisha kituo cha magari ya abiria au kushusha au kupakia abiria au mizigo katika eneo ambalo halijatengwa au kutambuliwa kwa kupewa kibali na Halmashauri kwa ajili ya matumiiz kama kituo cha magari ya abiria.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**7**. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia eneo lolote ndani ya kituo cha magari ya abiria kwa ajili ya kutoza ushuru na kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Usafi wa mazingira

**8**.-(1) Mtu yeyote anayetumia kituo cha magari ya abiria atapaswa kutunza mazingira kwa kutotupa taka ovyo, kumwaga au kutiririsha maji, kuosha vyombo vya usafiri katika eneo lisilo rasmi isipokuwa katika eneo lililotengwa kwa matumizi hayo.

(2) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri atahakikisha kuwa anaweka chombo cha kutunza taka ndani ya chombo cha usafiri na kutupa taka hizo katika maeneo maalumu yaliyotengwa na Halmashauri.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya biashara kwa kupanga bidhaa chini, kuweka meza za biashara, kuweka vibanda vya biashara, kupika au kufanya biashara ya chakula ndani ya eneo la maegesho bila idhini ya Halmashauri.

Maeneo ya maegesho

**9**.-(1) Halmashauri itatenga maeneo ya maegesho kulingana na matumizi ya eneo husika kwa kuainisha maeneo ya umma na binafsi au taasisi.

(2) Halmashauri itaweka alama au michoro maalumu itakayoonesha au kuashiria maeneo ya maegesho ya vyombo vya usafiri.

(3) Mtu yeyote ambaye anakusudia kuanzisha eneo kwa ajili ya maegesho atatakiwa kuomba kibali kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii kutoka Halmashauri na atawajibika kulipia asilimia kumi ya makusanyo yanayopatikana kila mwezi.

(4) Halmashauri inaweza kutoa kibali kwa ajili ya maegesho katika maeneo maalumu kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii endapo mwombaji atalipa ushuru wa maegesho kwa kipindi cha kuanzia wiki moja.

(5) Mtu yeyote anaweza kulipia ushuru wa maegesho kwa jumla ya gharama za siku, wiki au mwezi kwa mkupuo na atapewa kibali maalumu kitakachomruhusu kuegesha katika eneo lolote lililotengwa na Halmashauri kwa maegesho bila malipo katika kipindi hicho.

(6) Maeneo ya maegesho yatafunguliwa kuanzia saa kumi na moja kamili alfajiri hadi saa kumi na mbili kamili jioni katika maeneo ya kawaida na kuanzia saa moja kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni katika maeneo ya fukwe za bahari.

(7) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (6), Halmashauri inaweza kubadili muda wa kufungua

au kufunga maegesho kulingana na mahitaji au hali halisi ya maeneo hayo.

(8) Halmashauri inaweza kufunga maegesho kwa ajili ya matengenezo au sababu nyingine yoyote kadri itakavyoona na itatoa taarifa ya maandishi kwa watumiaji au kuweka matangazo sehemu ya maegesho ya magari ya abiria.

(9) Mtu anayekusudia kuegesha chombo cha usafiri katika maegesho ya Halmashauri atapaswa kulipa ushuru wa maegesho kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika sheria ndogo inayosimamia masuala ya ada na ushuru katika Halmashauri.

Uondoaji na uvutaji wa vyombo vya usafiri katika maegesho yasiyo rasmi

**10**.-(1) Itakuwa marufuku kuegesha chombo chochote cha usafiri katika maeneo yasiyotengwa kwa ajili ya maegesho au kuegesha kwa namna isiyoruhusiwa.

(2) Halmashauri itamchukulia hatua dereva au mtu yeyote atakayeegesha vibaya chombo cha usafiri au kuegesha katika eneo lisiloruhusiwa ikiwa ni pamoja na kufunga mnyororo au kifaa maalum kwenye chombo cha usafiri kilichoegeshwa vibaya na kumtaka mmiliki au mtumiaji wa kituo kulipa faini kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(3) Chombo cha usafiri ambacho kitakuwa kimefungwa mnyororo au kifaa maalumu zaidi ya saa mbili bila ya kulipiwa, kitavutwa na kupelekwa kwenye eneo maalumu lililotengwa na Halmashauri kwa gharama za mmiliki wa chombo cha usafiri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

(4) Halmashauri haitahusika na uharibifu utakaotokea wakati wa uvutwaji wa chombo cha usafiri isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa na uzembe wa Halmashauri au watumishi wake.

(5) Chombo cha usafiri ambacho kitahifadhiwa katika eneo maalumu lililotengwa kwa muda wa siku

thelathini bila kukombolewa, kitahesabika kama kimetelekezwa.

(6) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita Halmashauri itapeleka maombi mahakamani ili kuiomba mahakama itamke kuwa chombo hicho kimetelekezwa na hivyo itoe kibali chombo hicho kiuzwe kwa njia ya mnada wa hadhara.

(7) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (6), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hiyo.

(8) Fedha zitakazopatikana kutokana na mauzo ya chombo cha usafiri kilichouzwa kwa mnada zitatumika kulipia ushuru unaodaiwa, pamoja na gharama za kukamata na fedha zitakazobaki zitarejeshwa kwa mmiliki au mwakilishi wake.

Magari yasiyotozwa ushuru wa maegesho

**11.** Halmashauri haitatoza ushuru wa maegesho kwa vyombo vya usafiri vifuatavyo:

(a) magari ya Serikali;
(b) magari ya Kibalozi;
(c) magari yaliyoegeshwa katika sehemu za ibada wakati wa ibada;
(d) magari yaliyo na vibali maalumu kutoka Halmashauri;
(e) magari yaliyoegeshwa katika maeneo ya maegesho wakati wa shughuli maalumu za kitaifa;
(f) magari ya Wabunge na Madiwani wa Halmashauri;
(g) magari yaliyoegeshwa katika maeneo ya makaburi wakati wa mazishi; na
(h) magari ya wagonjwa.

Makosa

**12**. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

(b) ataharibu kwa namna yoyote miundombinu ya barabara, kifaa, kamera za usalama au taa za barabarani katika maeneo ya maegesho au kituo cha magari ya abiria;

(c) ataegesha chombo cha usafiri katika maeneo yasiyoruhusiwa kwa ajili ya maegesho;

(d) ataingiza gari la kuzoa taka au kufanya kazi ya kukusanya taka katikati ya Jiji nyakati za mchana bila kibali cha maandishi kutoka Halmashauri;

(e) ataingia au kutumia kituo cha magari ya abiria pasipo kulipia ushuru husika;

(f) atalaza chombo cha usafiri, ataosha, atatengeneza au atafanya shughuli yoyote kwenye eneo ambalo halijatengwa kwa shughuli hiyo ndani ya kituo cha magari ya abiria;

(g) atachafua mazingira kwa kutupa taka ndani ya kituo cha magari ya abiria au atatupa taka kutoka kwenye chombo cha usafiri;

(h) atatumia lugha ya matusi, zenye kuleta uchochezi au za kubughudhi zinazohatarisha usalama na amani ndani ya kituo;

(i) ataghushi kibali kinachotolewa na Halmashauri;

(j) atashindwa kuingiza chombo cha usafiri katika kituo cha magari ya abiria; na

(k) atatenda jambo lolote kinyume cha Sheria Ndogo hii.

Adhabu

**13**. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kutenda kosa lolote kinyume cha Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha kosa

**14.** Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari kosa na kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na. 41 la 2017

**15**. Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Vyombo vya Usafiri na Uboreshaji wa Mapato ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2017 inafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9(3))*

KIBALI CHA KUANZISHA MAEGESHO

Kibali hiki kimetolewa kwa Bw/Bi:………………………………………………wa S.L.P……………….

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ameridhia Ndugu mtajwa hapo juu, kuanzisha maegesho katika eneo la…………………….kwa kipindi cha …………………………

TAMKO LA MWOMBAJI:

MIMI………………………………………………………nipo tayari kuzingatia masharti ya kibali hiki cha maegesho ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Nathibitisha kwa hiari yangu kuwa nimeelewa vema masharti ya kibali hiki.

Jina: …………………………… Saini …………………..Tarehe …………………

KWA MATUMIZI YA OFISI:

Mwombaji amelipa shilingi ……………..….. tarehe……….mwezi……….mwaka…………..
(Ambatanisha stakabadhi ya malipo na fomu hii)

Jina la Afisa aliyetoa kibali………………… Saini …………… Tarehe …………
Wadhifa ................................

Muhuri:………………………………

JEDWALI LA PILI

*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 9(4))*

KIBALI KWA AJILI YA MAEGESHO KATIKA MAENEO MAALUMU

Kibali hiki kimetolewa kwa Bw/Bi:………………………………………………wa S.L.P………………. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ameridhia Ndugu mtajwa

*Tangazo la Serikali Na. 82 (Linaendelea)*

hapo juu, kuegesha katika eneo la…………………….kwa kipindi cha siku/wiki/mwezi………………………… baada ya kulipia huduma hiyo.

TAMKO LA MWOMBAJI

MIMI……………………………………………………nipo tayari kuzingatia masharti ya kibali hiki cha maegesho ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Nathibitisha kwa hiari yangu kuwa nimeelewa vema masharti ya kibali hiki.

Jina: …………………………… Saini …………………..Tarehe …………………

KWA MATUMIZI YA OFISI

Mwombaji amelipa shilingi …………………………..
tarehe……….mwezi……….mwaka…………..
(Ambatanisha stakabadhi ya malipo na fomu hii)
Jina la Afisa aliyetoa kibali……………………… Saini ……… Tarehe …………
Wadhifa ......................................

Muhuri:…………………………………

JEDWALI LATATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10(2))*

TOZO KWA AJILI YA MAEGESHO YASIYO RASMI NA KULAZA VYOMBO VYA USAFIRI

| Namba | Aina ya chombo cha usafiri | Tozo ya maegesho yasiyo rasmi (Shilingi) | Tozo ya kulaza chombo cha usafiri kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Bajaji au pikipiki | 50,000/= | 20,000/= |
| 2. | Gari dogo lenye uwezo wa kubeba uzito chini ya tani 2 | 50,000/= | 20,000/= |
| 3. | Gari lenye uwezo wa kubeba uzito wa tani 2 hadi 4 | 120,000/= | 20,000/= |
| 4. | Gari lenye uwezo wa kubeba uzito wa tani 4 na kuendelea | 200,000/= | 30,000/= |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10(3))*

USHURU WA KUONDOA NA KUVUTA CHOMBO CHA USAFIRI

| Namba | Aina ya Chombo cha Usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa la abiria | 300,000/= |
| 2. | Basi dogo la abiria | 200.000/= |
| 3. | Teksi | 80,000/= |
| 4. | Gari dogo binafsi | 70,000/= |
| 5. | Malori na Matrela zaidi ya tani 3 hadi 7 | 300,000/= |
| 6. | Malori na Matrela tani 7.1 na zaidi | 400,000/= |
| 7. | Gari la mizigo | 80,000/= |
| 8. | Pikipiki | 10,000/= |
| 9. | Bajaji | 50,000/= |

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 14)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwamba tarehe .......... ya mwezi .................. mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya …….. ya Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Vyombo vya Usafiri ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2025.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, NINAKUBALI kulipa kiasi cha shilingi.....................kama faini ya kufifilisha kosa na kiasi cha shilingi .....................ambacho ni ada au ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: .....................................................
Saini: ....................................................

MBELE YA MKURUGENZI:
Jina……...............................................
Saini: ..................................................
Tarehe: ...............................................

*Tangazo la Serikali Na. 82 (Linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya Jiji la Dar salaam imegongwa kwenye Sheria ndogo hizi kufutia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar esalaa uliofanyika tareha 06 Mwezi Machi Mwaka 2023 na kushuhudiwa lakari hiyo ikigongwa mbele ya:-

JAMAARY MRISHO SATURA,
*Mkurugenzi wa Jiji,*
*Halmashauri ya Jiji,*
*Dar Salaam*

MHE OMARI KUMBILAMOTO,
*Mstahiki Meya*,
*Halmashauri ya Jiji*
*Dar Salaam*

**NAKUBALI,**

L.S

Dodoma,
29 Agositi ,2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*